# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANANIA
# OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI
# MTAPIKA SECONDARY SCHOOL

Head office,
P. O. Box383,
**Masasi.**

"**TAALUMA, NIDHAMU NA KAZI**"
**IS OUR MOTTO**

Email: mtapikasecondary@gmail.com

Mkuu wa Shule: 0787193529
Makamu Mkuu wa Shule: 0713356133
Taaluma: 0710774811

Tarehe……………….

**Jina la Mwanafunzi**……………………………………..……….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MTAPIKA HALMASHAURI YA MJI MASASI MKOA WA MTWARA MWAKA………………..**

1. **0:** Kwaniaba ya kamati ya uchaguzi ninayo furaha kukuarifu rasmi kwamba umechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha **tano** Tahasusi ya ……….. mwaka………….. **TAALUMA, NIDHAMU NA KAZI**" maneno hayo ndiyo **KAULI MBIU** au mwongozo wa shule yetu. Ukiwa umekubali kujiunga na shule hii basi huna budi kuitafakari kauli hiyo. Shule ya Sekondari ya Mtapika ipo umbali wa kilometa tano na nusu kuelekea barabara yaTunduru kutoka stendi kuu ya mabasi Masasi mjini.Usafiri kutoka stendi kuu ya mabasi Masasi mjini kuja shuleni unapatikana kwa nauli ya Tsh. 2,000/= kwa pikipiki na kwa bajaji Tsh. 4,000/=. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe**………………..** Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe………………..na mwisho wa kuripoti ni tarehe……………………..

**2.0: Mambo muhimu ya kuzingatia**

2. **1: Sare ya shule**

(a) Sare za darasani ni:
- Suruali nyeusi mbili (kitambaa kizito) za heshima **ZISIWE** za kubana (modo).
- Shati nyeupe mbili za mikono mirefu na **ZISIWE** za kubana.
- Tai ndefu nyeusi.
- Viatu vyeusi jozi mbili vya ngozi vyenye kufunga gidamu.
- Soksi nyeupe jozi mbili.
- Sweta, rangi ya bluu.
- Raba nyeusi, jozi moja, bukta, rangi ya bluu na t-shirt rangi ya bluu kwa ajili ya michezo.
- Track Suit, rangi ya bluu.

(b) Sare za kushindia; ni suruali, rangi ya ugolo (aje nayo kutoka nyumbani). Na fulana rangi ya kijivu . (kwa gharama ya Tsh 15000/=).

**Muhimu**:
**Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa shuleni. Aidha mwanafunzi anaposafiri Kuja shuleni avae sare ya shule.**

2. **0: Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| 5 | **Jumla** | **80,000/=** |

**3. 1: MUHIMU:**

- Ulipaji wa michango yote ufanyike kwa njia ya Benki (**NMB**)
  Jina la akaunti ni **MTAPIKA SECONDARY SCHOOL.**

- **Michango** ilipwe kwenye **ACCOUNT No.70510045211.**

- Usisahau kuandika jina kamili la Mwanafunzi. Risiti (pay slip) iletwe kwa Mhasibu siku ya kufungua shule, **(mara tu mwanafunzi anaporipoti shuleni).**

- **BIMA YA AFYA-** Wanafunzi wote wenye bima waje nazo siku ya kuripoti na wasio na bima wana fursa ya kupata bima ya NHIF kwa gharama ya Tsh 50,400/= pesa hiyo iwekwe kwenye account no **70510045211.** Jina la akaunti ni **MTAPIKA SECONDARY SCHOOL.**
  **Angalizo** ; Bima hiyo ni kwa kipindi cha mwaka mmoja.

**3 2: Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni**

i. Madaftari 10 caunter book, kalamu na mkebe wa hesabu
ii. Shuka mbili rangi ya bluu, blanket 1, foronya 1, chandarua 1 nyeupe
iii. Ream 2 ya karatasi (Size A4) kwa mwaka
iv. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (Orodha imeambatanishwa)
v. Scientific calculator kwa wanafunzi watahasusi ya HGE HGK na HGL.
vi. Godoro la futi $2\frac{1}{2}$ftx4
vii. Taulo ,Mswaki, Dawa ya meno, Sabuni ya kufulia na kuogea.
viii. Nakala ya hati ya Matokeo kidato cha iv au"Result slip".
ix. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
x. Vyombo vya chakula[Sahani,Bakuli,Kijiko na Kikombe]
xi. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko na kikopo cha kuogea

**VIFAA VYA USAFI AMBAVYO MWANAFUNZI ANATAKIWA AJE NAVYO**:

(a) Wanafunzi wote wanatakiwa kuja na taa inayotumia solar au betri ya kutumia pale inapotokea dharula ya kukatika kwa Umeme.

(b) Vifaa vifuatavyo viletwe kulingana na TAHASUSI kama ilivyo katika jedwali,

| TAHASUSI | VIFAA |
|---|---|
| HGK | Dawa ya chooni ya maji lita5 ,fagio ya kawaida ya wima ya kufagilia nje ,jembe lenye mpini ,file1 ,hard broom ya kusafishia choo,nabafu. |
| HGL | Dawa ya chooni ya maji lita5 ,fagio yakawaida ya wima ya kufagilia nje,soft broom ya kufagilia ndani fyekeo,file1,. |
| HGE | Dawa ya chooni ya maji lita5 ,fagio ya kawaida ya wima ya kufagilia nje ,fyekeo ,mopa za kukaushia maji na file1. |

**3;4 SHULE YA SEKONDARI MTAPIKA**
**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

i. Heshima kwa viongozi ,Wazazi,Wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa. mipaka

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote,
vi. Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya Shule.
vii. Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za Shule.
x. Nimarufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari:na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU**;

-Mwanafunzi hapaswi kuja na **simu** shuleni kwa namna yeyote ile,nahakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.

-Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa . Nimarufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa .Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.

- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule.(Msiba au Ugonjwa)

**4.0: MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa Zaidi ya siku 90 bila taarifa/Utoro
iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,waalimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya
viii. Uvutaji wa sigara
ix. Uasherati,mahusiano ya jinsi moja,kuoa au kuolewa
x. Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sharia za nchi.
xi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni
xii. Kumiliki,kukutwa au kutumia **simu** ya mkononi katika mazingira ya shule
xiii. Kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

Fomu hii ya kujiunga na shule inatakiwa irudishwe ofisini pamoja na cheti cha kupima afya kilichojazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali ambacho pia kimeambatanishwa .Hakikisha umetoa nakala ya fomu hii kwa ajili ya rejea yako.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**MKUU WA SHULE**

**NB:Kwa siku za hivi karibun ikumekuwa na utapeli(Wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na Watu wanao jitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa watoto wa Mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NIVEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

- **MKUU WA SHULE:0787193529**
- **MAKAMU MKUU WA SHULE:0713356133**
- **MWANDAMIZI TAALUMA:0710774811**

**Mtapika Secondary School,**
**P.O.Box 383,**
**MASASI**

**Ref.No.……………………………….** **Date……………………**

**PARTA:**
**To the Medical Officer,**
**……………………………………….**
**……………………………………….**
**……………………………………….**

**REF:**……………………………………………………………………………….
Please examine the above named student as to his physical and mental fitness for being a student.Each defect will hinder a boy for Secondary School Education.

1.(a)Eyesight
(b)Hearing
(c)Limbs
(d)Speech
(e)Venereal Disease
(f)Leprosy
(g)Epilepsy
2.Neurosis
3.Otherseriousdiseases

**PARTB:MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by a GOVERNMENT MEDICAL OFFICER):
I have examined the above named student and consider that he is physically fit/not fit for a full time Secondary School Education.

(a) Eyesight………………………………(f)Leprosy……..................................
(b) Hearing……………………………….(g)Epilepsy………………………….
(c) Limbs…………………………………(h)Neurosis………………………….
(d) Speech…………………………………(i)Other serious disease……………..
(e) Venereal diseases…………………….

**Date…………………………..Signature………………………………**

**Station……………………Designation………………………….**

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1.Jina Kamili…………………………………………………………………………
(kama lilivyo kwenye selfform)
2.Tarehe ya kuzaliwa………………………………………………………….....
3.Anwani ya nyumbani…………………………………………………………………
4.Mahali unapoishi(nyumbani kwenu):Wilaya………….....Tarafa……………….
Kata…………………………Kijiji……………………………………………….
5.Shule ya sekodari uliyotoka………………………………………………………
6.Dini…………………………………………………………………………...
7.Kabila……………………………………………………………………...
8.Taifa(Mtanzania/SiMtanzania)……………………………………………...

PICHA

**9.Jamaa katika familia(Watakaohusishwa katika malezi ya mwanafunzi akiwa hapa shuleni)**

(i)Jina la Baba…………………………………………………………...
Anuani………………………………Namba ya simu……………………..
Anaishi/Haishi………………………………………………………...
Kazi yake………………………………………………………………...

PICHA

(ii)Jina la Mama………………………………………………………….
Anuani………………………………Namba ya simu……………………..
Anaishi/Haishi………………………………………………………...
Kazi yake………………………………………………………………...

PICHA

(iii)JinalaMlezi/Ndugu……………………………………………………….
Anuani………………………………Namba ya simu……………………..
Anaishi/Haishi………………………………………………………...
Kazi yake………………………………………………………………...

PICHA

**10.Mkataba wa Mwanafunzi kutoshiriki katika migomo,fujo na makossa ya jinai**

Mimi…………………………….(Mwanafunzi)na kirikuwa ,nimezisoma sheria,kanuni nataratibu za shule kwa umakini na utulivu mkubwa. Hivyo basi ninaahidi: “Nitazifuata Sheria ,Kanuni na Taratibu za shule kama zilivyoelekezwa Aidha ninaamini kuwa Sheria na Taratibu zipo kwa nia ya kunisaidia katika Nyanja zote muhimu ikiwa ni pamoja na nidhamu,maadili na taaluma.”Vilevile naahidi kuwa sitoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.Kinyume na hivyo hatua stahiki za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu.

……………………………..                ……..……...…………
Sahihi ya mwanafunzi                Tarehe

**11.Fomu ya Mzazi/Mlezi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yaliyotolewa na shule**

Mimi……………………………(Mzazi/Mlezi)wa Mwanafunzi…………………..Ninakiri kuwa,nakubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yote yaliyotolewa na shule.Hivyo basi niko tayari mtoto wangu asome katika shule hii nitakuwa tayari kumpa kila aina ya msaada utakaohitajika katika kufanikisha masomo yake namalezi yake kwa ujumla akiwa hapa shuleni kwa kipindi cha miaka miwili(2).

| | |
|---|---|
| …………………………….. | ……...………………… |
| Sahihi ya Mzazi/Mlezi | Tarehe |

**ORODHA YA VITABU (NUNUA KULINGANA NA MASOMO YAKO)**

**1.BASIC APPLIED MATHEMATIC ( HGE )**

- **BASIC APPLIED MATHEMATICS FOR ADVNCED SECONDARY SCHOOLS STUDENTS BOOK FORM FIVE AND SIX. TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION**

**2.ENGLISH LANGUAGE**

- **ENGLISH FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS.TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION.**
- **ANIMAL FARM.GEORGE ORWELL**
- **CHASING THE LEOPARD FINDING THE LION. JULIE WAKEMAN LINN**
- **THE OPPORTUNIST ELLITE. NYAMBARI C.M NYANGWINE.**
- **THE HORIZON UNVAILED. FELLOWES MWAISELA**
- **THE GOVERNMENT INSPECTOR. NIKOLAI V. GOGOI**
- **AN ENEMY OF THE PEOPLE. HENRIK IBSEN**
- **A TASTE OF HEAVEN. FAROUK TOPAN.**
- **SUMMONS: POEMS FROM TANZANIA. RICHARD S. MABALA et al.**
- **POETS OF AFRICA: LAMENT OF THE SILENT AND OTHER POEMS. JARED ANGIRA.**

**3.HISTORY**

- **HISTORY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS. STUDENTS BOOK FORM FIVE. TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION**

**4.KISWAHILI**

- **KISWAHILI SHULE ZA SEKONDARI KITABU CHA MWANAFUNZI KIDATO CHA TANO.TAASISI YA ELIMU TANZANIA**
- **UMAHIRI KATIKA NADHARIA YA LUGHA KISWAHILI (1) MASWALI NA MAJIBU KITABU CHA TANO NA SITA. CHACHA S.M**
- **DUNIA UWANJA WA FUJO. EUPHRASE KEZILAHABI**
- **UA LA FARAJA. W.E MKUFYA**
- **MIRATHI YA HATARI. C.G.MUNG'ONG'O**
- **WASIFU WA SITI BINTI SAAD.SHAABAN ROBERT**
- **MUKWAVA WA UHEHE.M.M.MULOKOZI**
- **SHUJAA MIRAMBO.EMMANUEL MBOGO**
- **USALITI MJINI.FRANCIS IMBUGA**
- **FUMBO LINALOELEA.NYAMBARI C.M.NYANGWINE**
- **MALENGA WA ZIWA KUU.WALLAH BIN WALLAH**
- **ANDAMO , MSAFIRI SAFARINI.MOHAMMED KHELEF GHASANI**
- **WOSIA WA BABA.AHMED MOHAMED AMANZY.**
- **VUTA N'KUVUTE.SHAFI ADAM SHAFI**
- **ASALI CHUNGU.SAID AHMED MOHAMED**
- **MWANA WA YUNGI HULEWA.MOHAMMED SAID ABDULLA.**
- **VIPULI VYA FIGO.EMMANUEL MBOGO**

**5.GEOGRAPHY:**

- **PHYSICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS. STUDENTS BOOK FORM FIVE AND SIX.TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION.**
- **PRACTICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS. STUDENTS BOOK FOR FIVE AND SIX.TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION.**
- **KITABU CHA RAMANI** (MAP SHEET).

**6.ECONOMICS:**

- **MACRO ECONOMICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS ,STUDENT'S BOOK FORM FIVE. TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATIONION**

**7. ACADEMIC COMMUNICATION**

- **ACADEMIC COMMUNICATION FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS STUDENTS BOOK FORM FIVE.TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION.**

**8.HISTORIA YA TANZANIA MAADILI**

- **HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI SHULE ZA SEKONDARI KITABU CHA MWANAFUNZI KIDATO CHA TANO. TAASISI YA ELIMU TANZANIA**